Patanishwa, Hesabiwa Haki, Takaswa

na

Ellis P. Forsman

Patanishwa, Hesabiwa Haki, Takaswa

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 14, 2011

Patanishwa, Hesabiwa Haki, Takaswa

Rumi.6:17-18

Wote tumetenda dhambi. Adamu na eva walileta dhambi ulimwenguni (Mwanzo 3). Tokea hapo wote wametenda dhambi.

- Rumi 3:14, *"Kama ilivyoandikwa, Hakuna mwenye haki, hakuna, hata mmoja."*
- Rumi. 3:23, *"Kwa maana wote wametenda dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;"*

Tumepatanishwa

Kwa nini tunahitaji kupatanishwa na Mungu.

Kwa sababu dhambi humtenganisha mtu na Mungu. Yoh. 9:31, "*Basi tunajua kuwa Mungu hawasikii wenye dhambi, lakini mtu yeyote akiwa muabudu Mungu, na kufanya mapenzi yake, huyo anamsikia."*

Mshahara wa dhambi ni mauti (kutenganishwa umilele kutoka kwa Mungu hadi motoni). Rumi. 6:23, *"Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti, bali karama ya Mungu ni uzima wa milele kupitia Yesu Kristo Bwana wetu."*

Huu upatanisho unawezekanaje?

Dhambi inamweka mtu mbali na Mungu. Tunahitaji kuwa mbali na dhambi**.**

Katika kuongoka kwetu tunaacha na dhambi.

Tuna batizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Matend. 2:38, *"Petro akawambia, tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."*

Tuna usulubisha utu wa kale wa dhambi, unazikwa katika ubatizo, na kuleta utu mpya wa kiroho katika Kristo. Rumi. 6:1-6, "*Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi? Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaungana kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, yakuwa utu wetu wa*

kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena."

Paulo anaiweka wazi kwamba katika mpangilio huu tunawekwa huru kutoka dhambini.

Rumi. 6:17-18, "*Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki."*

Dhambi imekwenda, Mungu atatu tunukia- tunapatanishwa kwa Mungu.

Tunahesabiwa haki

Dikaioo (dik-ah-yo-o) Kiyunani, kamusi ya Strong # 1344 — kufanya iwe na nguvu, kusamehe, kuthibitisha, kuimarisha.

Muumini aliye *"habiwa haki"* anahesabiwa kuwa na haki katika Yesu Kristo, na anakubaliwa katika kuwa ndani ya haki yake. *"Kuhsabiwa haki huku"* inaonyesha kwamba huduma ya Mungu kwa mwenye dhambi ni sawa na kwamba hajawai kutenda dhambi sasa kwamba anachukuliwa binafsi kuwa na haki katika Kristo Yesu.

Tunahesabiwa haki kwa neema ya Mungu. Rumi. 3:24, "*Wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu."*

Mtu lazima atii neema. Tito 2:11-12, *"Maana* ***neema ya Mungu iwaokoayo*** *wanadamu wote imefunuliwa; nayo yatufundisha kukataa ubaya na tama za kidunia; tupate kuishi kwa kiasi, na haki, na utauwa, katika ulimwengu huu wa sasa."*

Dhambi ikitoka tunapatanishwa kwa Mungu na kuhesabiwa haki- inafanywa kuwa sahihi.

- Rumi. 5:1, *"Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe imani kwa Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo."*
- Rumi.5:9, "*Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye."*
- 1 Wakor. 6:11, *"Na baadhi yenu mlikuwa watu wa namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu Kristo, na katika Roho wa Mungu wetu."*

Tunatakaswa

Utakaso (Hagiasmos; Kiyunani; Kamusi ya Strong # 38)- kazi ya Roho Mtakatifu kuwaweka watu pembeni katika wokovu na kumuwezesha awe mtakatifu kama jinsi Mungu alivyo mtakatifu.

Kristo alipojitakasa (Yohana 17:19), anamaannisha alijiweka wakfu katika kazi yake kama mkombozi.

Yohana 17:19, "*Na kwa ajili yao najiweka wakfu mwenyewe, ili na hao watakaswe katika kweli."*

Neno "takatifu" inatoakana na chimbuko na inamaanisha "mtu aliyetakaswa"- mtu aliye wa Kristo.

Hili neno rasmi inatokea katika 1 Wakor. 7:12-14, ambapo mwanaume asiyeamini inasemekana atakaswe na mkewe, haimaanishi kwamba yuko tofauti na tabia ya kawaida, bali anasimama katika hatua Fulani na Mungu.

1 Wakor. 7:12-14, *"Lakini watu wengine nawambia mimi, wala si Bwana, ya kwamba iwapo ndugu mmoja ana mke asiyeamini, na mke huyo anakubali kukaa naye, asimwache. Na mwanamke ambaye anamume asiyeamini, na mume huyo anakubali kukaa naye asimwache mumewe. Kwa maana yule mume asiyeamini hutakaswa katika mkewe, na Yule mke asiyeamini hutakaswa katika mumewe, kama isingekuwa hivyo watoto wenu wangekuwa si safi, bali sasa ni watakatifu."*

Sasa kwa vile sisi tu wake Kristo tunapaswa kuishi kwake.

- Waef. 4:1, "*Kwa hiyo nawasii mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustaili wito wenu mlioitiwa."*
- Wakol. 3:1-4, *"Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu. Kristo atakapofunuliwa, aliye uha wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu."*
- 1 Wathes. 5:10, *"Ambaye alikufa kwa ajili yetu, ili tuishi pamoja naye, kwamba twakesha au kwamba twalala."*

Hitimisho

Je umeshatakaswa kupitia ubatizo? Yafuatayo ni hatua mhimu ili uweze kupatanishwa na Mungu na kuhesabiwa haki na Yesu Kristo kwa tukio hilo:

- **Imani.** Waeb. 11:6, *"Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza, kwa maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko, na kwamba huwapa dhawabu wale wote wamtafutao."* Nilipokuwa shuleni (nikiwa na miaka 17), kijana mmoja jirani yangu mwaka sawa na wangu aliniambia kwamba haamini kwamba Mungu yupo. Kwa vile nilikuwa nimeshabatizwa, nilichukua nafasi ya kuongea naye kuhusu maandiko. Akaniambia kuwa anaona kuishi maisha ya ukristo ni nzuri, lakini hakuwa na uhakika kwamba Mungu yupo. Lakini ilikuwa sehemu salama, labda anaweza kwenda kanisani, na atakapokufa na kusimama mbele za Mungu (kama kuna Mungu) siku ya hukumu (kama kuna hukumu), labda Mungu akiona kwamba amekwenda kanisani na akaishi maisha mazuri Mungu atampeleka mbinguni (kama kuna mbingu), na siyo motoni (kama kuna moto). Nikamwambia, "haiendi hivyo. Lazima umwamini kwa moyo wako wote lasivyo huwezi kumpendeza."

- **Toba.** Matendo. 2:38, *"Petro akawambia, tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu katika jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* Matend. 11:18*, "... Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao <u>toba liletalo uzima .</u>* wakati ulipokuwa unalala, ukasikia kelele katika chumba kingine, na ukafikiria mwenyewe, "kuna mwizi ndani ya nyumba!" kwa hiyo ukachukua simu ya mkononi, na kwa haraka ukawapigia polisi, ukiwambia kuna mwizi ndani kwako, na ukawapa namba ya nyumba yako. Muda mfupi ukasikia wanafika na wanamashika mwizi. Mwizi akapiga kelele, "samahani; anaomba msamaha juu ya nini? Anaomba msamaha kwa sababu ameshikwa; na siyo kwamba ameiba. Katika toba ya kweli mwizi angeomba msamaha kwamba hataiba tena. Hiyo ndiyo toba ya kweli. Ni badiliko la nia linaloleta badiliko la matendo. Hiyo ndiyo tunatakiwa tufanye kabla hatujawa Wakristo.

- **Kukiri.** Rumi. 10:9-10, *"Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana <u>kwa moyo mtu huamini hata kupata haki</u>, na <u>kwa kinywa hukiri hatakupata wokovu."</u>* Yesu Kristo ni mwana wa Mungu.

Kumbuka kwamba katika andiko hilo hapo juu imani (Kuamini), kutubu na kukiri ni "**KATIKA"** haki, maisha, au wokovu. "Katika" inamaanisha kuelekea kitu Fulani; siyo kwamba mtu ameshapata.

- **Batizwa.** Ni katika ubatizo tu ambapo haki, maisha, na wokovu unapatikana. Yesu, mwenyewe, alibatizwa kutimiza haki yote, *"Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, kubali hivi sasa kwakuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini, na tazama mbingu zika mfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, Huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninaye pendezwa naye."* Yesu alibatizwa kwa sababu Mungu alisema ni jambo zuri kufanya. Unaona ni jinsi gani ilimpendeza Mungu baada ya Yesu kubatizwa? Yesu pia akasema *"imekuwa* ***kwetu*** *kuitimiza haki yote."* Tunabatizwa kwa sababu inatimiza haki yote, si kwa sababu ni kwa ajili ya haki yetu.

  Kwa kweli, tusipobatizwa, bado tupo katika dhambi. "*Petro akawambia, tubuni, mkabatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu Kristo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, na mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."* (Matend 2:38). Petro, umesema ubatizo ni kwa ajili ya nini? *"kwa ajili ya ondoleo la dhambi".* Kwa nini watu wanaacha hatua inayotuondoa dhambi?

  Yesu aliamuru kuwa ili tuufikie wokovu ni lazima tubatizwe. *"Akawaambia enendeni ulimwenguni mwote mkahubiri injili kwa kila kiumbe. Aaminiye* ***na*** *kubatizwa ataokoka; asiyeamini atahukumiwa."* (Marko 16:15-16).

  Anania alimwambia Sauli (kabla hajaitwa Paulo) kitu hicho icho, "*Sasa unakawilia nini? Simama, na ubatizwe na uoshwe dhambi zako, huku ukiliitia jina la Bwana."* (Matnd. 22:16). Ubatizo ni hitaji lililotolewa na Mungu.

  Ubatizo unaitwa maziko. "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima."* Utuwetu wa kale lazima ufe ndani yetu. *"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika*

mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili ya kuwa utuwetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye ili mwili wa dhambi ubatilike tusitumikie dhambi tena." (Rumi. 6:3-6). Ubatizo ni ramani ya Mungu inayotumika katika damu ya Yesu Kristo ndani ya maisha yetu kwa ubatizo. Tunakuwa huru katika dhambi zetu za zamani pale tu tunapo batizwa.

Hii hai maanishi "kunyunyiza. Andiko hilo juu inasema ubatizo ni maziko. Hatu peleki maiti makaburini na kuweka udongo kidogo juu yake; tunazika mwili.

Kama hujawa mkristo, kwa nini usifanyike leo?